



**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Sita – Tarehe 12 Mei, 2021.**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi  
na Dua itasomwa.

**I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa Mwaka 2021/2022.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka 2021/2022.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC):**

Hotuba ya maoni ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) kuhusu Hotuba ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora (Bajeti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali) kwa Mwaka 2021/2022.

## **II. MASWALI:**

### **Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

98. MHESHIMIWA MWANAASAHA KHAMIS JUMA (Jimbo la Dimani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Eneo la Fumba limebahatika kuwa sehemu ya uwekezaji hapa nchini. Hata hivyo, kuna changamoto katika uwekezaji huo kwa wananchi ikiwemo mipaka ya maeneo ya matumizi ya ardhi kwa wawekezaji pamoja na wananchi wa eneo la Fumba.

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kubainisha kwa uwazi na kuwaeleza wananchi mipaka halisi ya eneo la uwekezaji na maeneo ya matumizi kwa ajili ya wananchi.
- (b) Kutobainishwa kwa mipaka hiyo ya maeneo ya uwekezaji na yale ya matumizi ya wananchi, Je, Serikali haioni kuwa kunaweza kupelekea migogoro ya ardhi isiyokuwa ya lazima.
- (c) Wananchi wa Fumba wategemee lini utafanyika mpango huo wa kubainisha kwa uwazi mipaka hiyo.

### **Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

6. MHESHIMIWA SHAABAN ALI OTHMAN (Jimbo la Mpendae)

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kumekuwa na ahadi ya muda mrefu sana ya ujenzi wa barabara ya Mpendae inayotoka Kwa Mchina hadi skuli ya Jang'ombe ambayo hata aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mpendae Marehemu Salim Abdalla Turkey aliwahi kutoa fedha taslim shilingi milioni 100 ili kusaidia ujenzi huo.

- (a) Je, Serikali inalifahamu kwa kiasi gani suala hili.
- (b) Ni sababu gani za msingi na za kitaalamu zilizosababisha kukwama kwa ujenzi wa barabara hiyo.
- (c) Je, Serikali inatoai ahadi gani ya kuijenga barabara hiyo.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

86. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR HASSAN (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Inaonekana soko la kununua karafuu Zanzibar limeshuka kwani kuna karafuu ambazo zimechumwa tokea kipindi kilichopita na bado hazijauzwa, hali inayosababishwa na uhaba wa fedha wa Shirika la ZSTC.

- (a) Je, ni lini soko la karafuu litakuwa tayari ili wananchi wauze karafuu zao kabla ya msimu mwengine kuanza.
- (b) Kama soko limeshuka, Je, Wizara inawaahidi nini wananchi waliochuma karafuu kwa gharama katika awamu iliyopita.

**III. HOJA ZA SERIKALI:**

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa mwaka 2021/2022.

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka 2021/2022.

Zanzibar,  
12 Mei, 2021.

(Raya Issa Msellem)  
**KATIBU WA BARAZA**